# HOTUBA YA MHESHIMIWA WAZIRI WA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO.

# MHE. RIZIKI PEMBE JUMA (MBM) KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA, TAREHE 16/06/2023 KATIKA UKUMBI WA SHEIKH IDDRISA ABDUL WAKILI – KIKWAJUNI.

**Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maendeleo ya Jamii,**

**Ndugu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii,**

**Ndugu Wakurugenzi Mbalimbali Mliopo kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Wizara nyengine,**

**Ndugu Wawakilishi wa Mashirika mbalimbali ambao tumeungana katika kuandaa Shughuli hii ikiwemo Save the Chilren, C-SEMA, PATHFINDER, Action Aid na ZCRF,**

**Ndugu Viongozi mbalimbali wa Mabaraza ya Watoto na Vilabu, Ndugu Walimu wa Skuli mbalimbali Mliopo,**

**Ndugu Maafisa wa Maendeleo ya Jamii Mliopo,**

**Ndugu Waalikwa Mbalimbali,**

**Ndugu Wazazi na Walezi Mliopo,**

**Ndugu Wandishi Wa Habari kutoka Vyombo Mbali Mbali,**

**Itifaki imezingatiwa.**

ASSALAMU ALEYKUM,

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kutukutanisha tena kwa mara nyengine tukiwa wazima. Pia napenda kuchukua fursa hii kukushukuruni washiriki nyote kwa ushiriki wenu katika shughuli hii ya leo kwani kuwepo kwenu ndio kufanikiwa kwa shughuli hii.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru taasisi zote ambazo zimekaa na kuwaza kuwa na shughuli hii siku ya leo kwa kushirikiana na Wizara Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika kuunga mkono kwa hali na mali katika kufanikisha maadhimisho ya siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka 2023.

Vile vile naishukuru kamati iliyoandaa Kongamano hili kwani kwa hakika limefana na limeonesha ni kwa kiasi tunawajali na kuwathamini watoto kwa kuyafanya mambo yetu kwa vitendo, nimedokezwa kwamba kamati hii ilikuwa imejumuisha taasisi zote ambazo zimejitoa kwa hali na mali kukamilisha azima hii zikiongozwa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii na Wasaidizi wake. Hongereni sana Kamati kwa ujumla wenu.

N**dugu Washiriki,**

Natambua kwamba  kila ifikapo tarehe 16 Juni ya kila mwaka ni siku ya Maadhimisho ya siku ya Mtoto wa Afrika ambayo yanafanyika katika nchi zote wanachama wa Umoja wa Afrika kwa namna tofauti. Wakati wa maadhimisho haya tunakuwa tukikumbuka watoto waliouawa kikatili Mjini SOWETO katika nchi ya Afrika ya Kusini mwaka 1976, wakipinga ubaguzi wa rangi na utumiaji wa Lugha ya Kikaburu (Africans) Maskulini, tumuombe mungu majanga kama haya yasitokee tena watoto wetu duniani kote. Niwapongeze Viongozi wote wa tasisi ambazo zimeandaa hafla hii kwa kufikiria hatua hii ya kuungana na mataifa mengine ya Afrika kwa lengo la kutaka kuijuilisha jamii umuhimu wa Mtoto na kuweka misingi ya kumlinda ili asiweze kupatwa na vikwazo vyovyote vilivyopo katika jamii yetu.

N**dugu Washiriki,**

Siku hii inatoa fursa kwetu kuweka misingi mizuri ya kuwalinda na kuwaendeleza watoto wetu ili kujenga kizazi bora na chenye kuzingatia maslahi yao. Pia inatupa  msukumo wa kuzidisha mashirikiano baina ya wazazi, walezi, sekta zinazowahudumia mama na mtoto pamoja na mashirikiano yetu na  wadau wa maendeleo katika kusimamia na kuitekeleza sheria Nam. 6 ya mtoto ya mwaka 2011, Zanzibar pamoja na mikataba ya kikanda na kimataifa inayohusu masuala ya mtoto.

N**dugu Washiriki,**

Kwa mwaka 2023 ujumbe wa siku ya Mtoto wa Afrika Kimataifa kwa Bara letu la Afrika ni **“The Rights of the Child in the digital environment”,** kwa kuzingatia muktadha /mazingira yetu ujumbe wa Kitaifa wa Zanzibar ni “**Muwezeshe na Mlinde Mtoto katika matumizi Sahihi ya Mtandao**” Ujumbe huu umekuja wakati muwafaka kwa kuyataka mataifa wanachama wa Umoja wa Afrika, wananchi pamoja na mashirika kuzingatia namna bora ya kutumia matumizi ya mtandao na kuweka mazingira mazuri bora na rafiki ya upatikanaji wa haki kwa watoto kupitia mitandao bila kuathiri ustawi wao wa maisha ya kila siku**.** Pia kuwalinda na kuwasimamia Watoto wasikumbane na changamoto zinazotokana na matumizi ya mtandao ikiwemo simu, mitandao ya kijamiii kama vile facebook, Tiktolk, Whatsap, Instagram, Snapshat, na mengineo. Uwezeshaji na Ulinzi wa mtoto ni maeneo kipekee ya kumuandaa mtoto kuwa raia mwema wa baadae na rasilimali ya taifa katika ujenzi wa Jamii mpya katika harakati za kukuza maendeleo ya uchumi na kijamii nchini. Hivyo ni vyema kuzitumia nyezo na rasilimali hizo kwa ueledi mkubwa ili kuwekeza kwa Watoto wetu.

N**dugu Washiriki,**

Takwimu za utafiti uliofanywa mwaka 2022 kupita Mradi wa “ **The Disrupting Harm Project”** na taasisi ya End Violence Agaist Children,

UNICEF, ECPAT, INTERPOL, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee na Makundi Maalumu -Tanzania Bara, Wizara neyngeine za Zanzibar pamoja na Taasisi nyengine zimeonesha kwamba asilimia 67% ya watoto wenye umri wa miaka 12-17 wamekuwa ndio watumiaji wakuu wa mitandao na Zanzibar wakiwa wamejumuishwa katika takwimu hizo. Pia imebainika kuwa kati ya asilimia 67% ya watoto wanaotumia mitandao kati ya hao asilimia 26% ni wasichana wenye umri wa miaka 12-13 wamekuwa watumiaji wa Mitandao licha ya kupata vizuwizi kutoka kwa wazazi wao. Aidha, wamekuwa wakibainisha kwamba kupitia utumiaji wa mitandao wamekuwa wakikutana na watu mbalimbali ambao hawawajui na kuzungumza nao kwa kushare nao picha zisizo na maadili au urafiki ambao baadae huleta madhara.

N**dugu Washiriki,**

Pamoja na hayo, ripoti hiyo imeendelea kuchambua na kubainisha kwamba takiribani asilimia 5% ya watoto wanaeleza kwamba waliwapata watu wasiowajua kupitia mitandao na kufurahishwa nao, asilimia 3% wamebainisha kwamba walishare picha za Ngono na Watu waliojuana kupitia Mitandao na ambao hawakuwa wakiwajua hapo kabla. Pia ripoti inaelezea kuwa asilimia 4% ya watoto wenye umri wa miaka 12-17 ambao ni watumiaji wa Mitandao walikuwa ni waathirika wa matendo ya Ukatili na Udhalilishaji kupitia Mitandao (Cyberbullying on Sexual violence through digital form) na Kutumikishwa kwa

kushawishiwa, kudanganywa na hata kutozwa Nguvu kufanya matendo hayo.

N**dugu Washiriki,**

Kutokana na changamoto hizo napenda kuchukua nafasi kuiasa Jamii kuacha kuwapatia watoto simu au kuwaruhsu kwenda kwenye vibanda ambavyo vinatoa huduma ya Internet or Free Wife kwa matumizi yasiyosahihi ili kudhibiti watoto wetu na Vitendo vya Udhalilishaji. Inatupasa kutafakari njia bora za kuilinda Jamii yetu hasa watoto ili kuwaweka katika mazingira ya usalama. "**Ulinzi wa Mtoto ni haki yake ; Muepushe na Ukatili kupitia Mitandao**". Tuwajibike kwa pamoja kuondoa tatizo la malezi holela ya watoto wetu ili kuwaepusha na matendo ya uonevu.

Wazazi tuweke passwadi zetu katika simu au Ipad zetu/ Kishikwambi pale ambapo kunauhitaji wa kumuachia mtoto wako ila kama sio lazima basi epuka kumuachia simu mtoto mtoto wako au kumruhusu kwenda masafa ya mbali akiwa na uhuru mkubwa.

N**dugu Washiriki,**

Malezi ya Pamoja ni Msingi unaijenga Jamii na kuliweka Taifa letu kuwa taifa lenye kuogopewa Kimaadili, nidhamu na hata kuthaminiwa na watu wengine kutoka na kushikama kwa pamoja. Tukumbuke ule usemi usemao "Kidole Kimoja Hakivunjia Chawa" ni dhahiri kwamnba usemi huu bado unatupa mazingatio ya kwamba tunaposhikama na tukawajibika katika kuwalea watoto wetu vyema basi hakuna adui atakaechafu mila, silka na maadili yetu kwa watoto wetu. Tuanze kuekeza kwa Watoto kila mmoja na tuaje kujisemea maneno "**Watoto**

**wa siku hizi**" usemi huu umepitwa na wakati kwani hakuna mtoto alieletwa na wakati ila wakati ndio unaotuelekeza ni mambo gani tunapaswa kuyafanya tukiwa na umri upi au maeneo yepi. Mfano ukiwa hujafikia Balenghe tunaelezwa kwamba huandikiwi dhambi. Hii ni kueshiria kwamba wakati na ukuaji wa kila mtoto ndio unaozingatiwa kwa matendo yao.

N**dugu Washiriki na Waandaaji wa Kongamano,**

Nichukue fursa hii kutoa rai kwenu pamoja na wizara yetu kushirkiana kufufua ile timu ya ufuatiliaji wa masuala ya Mitandao ambayo iliundwa Kitaifa kwa Tanzania lakini utendaji wake bado haujatuamsha vyema, nashauri tukao kwa pamoja na niiombe taasisi ya C-SEMA, Save the Children na SOS kuandaa mazingira ya kufufua Timu kama hii hapa Zanzibar ili kuendelea kufuatilia Maudhui Mtandaoni na kuendelea kuishari Wizara, taasisi zinazoshughulika na Watoto pamoja na kuandaa mikakati ya kukabailiana na tatizo la Watoto kujihusisha na Maudhui yasiyo rasmi katika Mitandao.

Aidha, kuwepo kwenu kunaweza kufungua milango ya kutatua changamoto hii ambayo Jamii yetu kwa sasa inakabiliana nayo. Ninamuomba Katibu Mkuu wangu Bi Abeida Rashid, Jembe langu kuandaa mazingira ya kuka na timu ya taasisi hizo na nyengine ili kuangalia mazingira bora ya kutatua changamoto hiyo. Vile vile,

tusisahu na kuwajumuisha na watoto wenyewe kupitia Bodi ya Ushauri ya Watoto (NCAB) Zanzibar.

N**dugu Washiriki,**

Mwisho naomba nimalize kwa kuwashuruninyote kwa kwa kujumuika na sisi ila nitakuwa mchoyo wa Fadhila kama sitoweza kuzishukuru taasisi zilizoshirikiana na sisi katika kuandaa Hafla hii, naomba nizitaje kwa uchache taasisi hizo ambazo ni Save the ChildreN, C-SEMA, PATHFINDER, ACTION AID, ZCRF, SOS na Wizara ninayoingoza kwa ujumla wake. Baada ya kuyasema hayo sasa naomba nitamke rasmi kwamba KONGAMANO LA MAADHIMISHO YA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA TAREHE 16 JUNI MWAKA 2023 NIMELIFUNGA RASMI.

**AHSANTE KWA KUNISIKILIZA.**

**MHESHIMIWA WAZIRI WA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO.**

**MHE. RIZIKI PEMBE JUMA (MBM)**